HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
SHULE YA SEKONDARI KIBWEHERI

Simu: 0684690133/0674766544
Barua Pepe: kibweheriss@gmail.com

S.L.P. 90113
DAR ES SALAAM

---

# FOMU YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA – 2023

JINA LA MWANAFUNZI___________________________________

Uongozi wa shule ya sekondari **Kibweheri** tunayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2023 shuleni hapa ukiwa mwanafunzi wa kutwa. Hongera na karibu sana.

**MAHALI SHULE ILIPO**.

Shule ipo mkoa wa **Dar es salaam**, Wilaya ya **Ubungo,** Kata ya **Kibamba,** Mtaa wa **Kibwegere,** kilomita **tano** (5) kutoka barabara kuu ya Morogoro upande wa Magharibi ( Kutokea kituo cha daladala cha Kibamba Njiapanda/Kibamba Shule).

**MUDA WA KUFUNGUA SHULE**

Shule itafunguliwa tarehe 09. 01. 2023 saa 1:00 asubuhi. Fika siku hiyo ukiwa na mahitaji yote ya shule ( kama yalivyoainishwa hapa chini) kwa ajili ya usajili. Zingatia kuwa mwanafunzi ambaye hataripoti kwa muda ulioelekezwa nafasi yake itachukuliwa na mwanafunzi mwingine aliyeikosa.

**MAHITAJI MUHIMU YA KUJA NAYO SHULE**

1. Sare kamili ya shule.
2. Begi la kubebea daftari na zana za kujifunzia
3. Mkebe wa vifaa vya Hisabati.
4. Daftari tisa (09) – {Counter book Quire 3 au 4}
5. Dictionary (Kamusi) ya “English – Kiswahili” au “English – English”.
6. Kalamu za wino, Penseli na Rula.
7. Faili la kutunzia nyaraka zenye taarifa muhimu za mwanafunzi.
8. T-shirt na bukta (rangi ya bluu) na raba kwa ajili ya michezo.
9. Ndoo ndogo ya Lita 10 kwa ajili ya matumizi binafsi ya mwanafunzi chooni.(Usalama wa Afya)

MAELEZO YA SARE YA SHULE

WAVULANA

A. Shati jeupe la mikono mifupi na LISILOBANA.
B. Suruali ya rangi ya KIJIVU (iliyoiva) yenye upana wa inchi 15½ (cm 39) chini na marinda mawili kila upande.( zingatia upana wa suruali chini utoshe kupitisha chupa ya soda.)
C. Soksi za rangi NYEUSI.
D. Viatu vyeusi vya kufunga kamba. VISIVYO NA KISIGINO KIREFU.

NB: NYWELE ZIWE FUPI (Siyo kipara)

WASICHANA

A. Shati jeupe la mikono mifupi na LISILOBANA.
B. Sketi ( Rangi ya KIJIVU (iliyoiva), yenye MARINDA, Inayovuka MAGOTI.

C. Soksi za rangi NYEUPE.
D. Viatu vyeusi vya kufunga kamba. VISIVYO NA KISIGINO KIREFU.

NB: NYWELE ZIWE FUPI ( Siyo Kipara).

# SHERIA ZA SHULE.

Nidhamu kwa ujumla

1. Ni lazima mwanafunzi awahi shuleni asubuhi saa 1:00 na kufanya usafi wa mazingira ya shule na kuhudhuria gwaride la ukaguzi wa usafi na kuchangamsha mwili
2. Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kuondoka katika eneo la shule bila kupata kibali kutoka kwa mwalimu wa darasa, wa zamu au idara ya malezi
3. Mwanafunzi anatakiwa kusimama, kusalimia na kuwapokea mizigo walimu au mtu yeyote mwenye umri mkubwa Zaidi yake popote pale akutanapo na mtu wa aina hiyo
4. Hairuhusiwi kutumia LUGHA CHAFU miongoni mwa wanafunzi na kwa mtu mwingine yeyote
5. Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wanafunzi wenzake, viranja na wafanyakazi wote wa shule
6. Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vya darasani na shughuli za michezo na uzalishaji mali kwa mujibu wa ratiba
7. Mwanafunzi lazima afanye mitihani ya masomo yote anayosoma shuleni hapa.
8. Mwanafunzi awapo shuleni haruhusiwi kuwa na aina yoyote ya vitu vifuatavyo:-
   Kucha ndefu, kupaka rangi, kuvaa cheni, heleni, nywele ndefu, kunyoa kipara, kunyoa nyusi kupaka dawa nywele n.k
9. Mwanafunzi ahakikishe kuwa awapo mahali popote ndani au nje ya shule awe amevaa nguo za heshima, ni marufuku kuvaa nguo zinazobana, fupi na nyepesi
10. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo Zaidi ya zile zilizotajwa katika maelekezo ya kujiunga na shule ikiwemo sweta la rangi inayotakiwa
11. Wanafunzi wanatakiwa kutunza mali zao binafi na mali za shule. Pia wanatakiwa kutoa taarifa juu ya uharibifu wa mali za shule
12. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kwenda kwenye maeneo yafuatayo bila sababu maalum au bila kupewa ruhusa:-
    i. Shule za jirani na madukani
    ii. Nyumba zinazozunguka shule
    iii. Vibanda vya biashara nje ya shule
13. Ni marufuku kwa mwafunzi kukutwa sehemu zifuatazo:-
    i. Baa na club za usiku
    ii. Nyumba za kulala wageni isipokuwa wanapokuwa na wazazi au walezi wao
14. Wawapo shuleni wanafunzi hawaruhusiwi kumiliki vitu vya gharama kama: simu ya mkononi, radio, kamera, ipad, albamu za picha na CD.
15. Kila mwanafunzi ni lazima afanye bidii katika kila somo. Mwanafunzi ambaye atapata chini ya 50% mwisho wa mwaka atapata adhabu kali.
16. Hakikisha ukimya wa hali ya juu unazingatiwa katika maeneo yote ya shule na kujifunzia hasa darasani, maktaba, maabara na kwenye korido wakati wa vipindi.
17. Adhabu ya viboko itaruhusiwa kwa kosa linalostahili na kuwa na taarifa/ kibali cha mkuu wa shule

18. Hakikisha muda wote unapokuwa shuleni unaongea LUGHA YA KIINGEREZA nje na ndani ya darasa
19. Mwanafunzi yeyote akikamatwa na kitu chochote kisichotakiwa shuleni kitaharibiwa mbele yake

**MAKOSA AMBAYO MWANAFUNZI AKIYAFANYA ANAWEZA KUFUKUZWA SHULE.**

1. Kutochukua ripoti ya maendeleo yake ya nusu mwaka au mwaka
2. Ulevi au matumizi ya madawa ya kulevya
3. Aina zote za wizi na unyang'anyi
4. Aina zote za makosa ya kujamiiana na uasherati. Hii ni pamoja na kukutwa na mikanda ya video, vitabu vichafu vya uasherati au vitu vinavyofanana na hivyo.
5. Kupiga au kupigana.
6. Matumizi ya lugha chafu au matusi.
7. Makosa ya jinai.
8. Kuzomea watumishi au kuchokoza wanafunzi wengine.
9. Kugoma au kuchochea mgomo (ghasia).
10. Kutohudhuria shuleni kwa muda wa siku 90 mfululizo.
11. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule (pia ikithibitika kutoa mimba)
12. Kuoa au kuolewa.
13. Kudharau bendera ya Taifa kwa kutohudhuria parade.
14. Kukuwadia mwanafunzi mwenzie au mtumishi yeyote katika mambo ya mapenzi ndani na nje ya shule
15. Kumnyanyasa mwanafunzi mwenzie kutokana na jinsia yake , udini, ulemavu, ugeni wake, au hali yake
16. Kughushi mitihani au wizi wa mitihani, kukataa au kutofanya mitihani na mazoezi ya masomo bila sababu za msingi
17. Kukataa adhabu kwa makusudi , pia adhabu inaweza kutolewa na mwalimu au kiranja yeyote kwa mwanfunziu anaeonesha utovu wa nidhamu
18. Kuharibu mali za shule ikiwa ni pamoja na majengo, mali ya mtu au kundi la watu.
19. Kukamatwa na simu, redio, kamera , ipadi , albamu za picha na CD kwa mara ya pili baada ya kuonywa kwa mara ya kwanza.

HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
SHULE YA SEKONDARI KIBWEHERI

**WAJIBU WA WAZAZI/WALEZI**

1. Mzazi/ mlezi anatakiwa kumleta mwanae kumwandikisha shuleni anapoanza masomo
2. Mzazi au ,mlezi anatakiwa kandika majina ya watu wanne na namba zao za simu watakaoruhusiwa kupata ripoti za mtoto akiwa shuleni na mawasiliano ya vikao, wito n.k
3. Mzazi au mlezi anatakiwa kuja kuchukua ripoti ya mtoto wake kwa muhula husika vinginevyo hatapokelewa muhula unaofuata
4. Mzazi/mlezi anatakiwa kufika shuleni kwa muda mwafaka pindi anapohitajika na uongozi wa shule
5. Mzazi/mlezi ajenge tabia ya kutembelea shule mara kwa mara ili kujua maendeleo ya mtoto wake badala ya kusubiri mwisho wa muhula, ili kujenga mshikamano wa malezi
6. Mzazi au mlezi amfahamu kwa jina na namba ya simu ya mwalimu wa darasa la mtoto wake ili kujenga mahusiano ya malezi ya mtoto.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YETU**

**……………………………………….**

**MKUU WA SHULE.**

HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
SHULE YA SEKONDARI KIBWEHERI

**KIAMBATISHO A**

**FOMU RASMI YA KUANDIKISHWA ( Ijazwe na Mwanafunzi)**

| MAJINA 3 YA MWANAFUNZI | URAIA | DINI | TAREHE-KUZALIWA | MAHALI ULIPOZALIWA | YATIMA ? Ndiyo/Hapana/Mzazi 1 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

**TAARIFA ZA SHULE YA MSINGI ULIYOSOMA. (Jaza Jedwali Hapa Chini).**

| SHULE YA MSINGI ULIYOMALIZA | MAJINA ULIYOANDIKISHWA SHULE | MWAKA ULIOANZA | MWAKA ULIOMALIZA |
|---|---|---|---|
| | | | |

Saini ya Mwanafunzi_________________________Tarehe__________________

**TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI (Ijazwe na Mzazi/Mlezi)**

| MAJINA 3 YA MZAZI/MLEZI | URAIA | ANUANI YA MAKAZI | | | | SIMU<br>1 Mzazi/mlezi<br>2 Jirani wa karibu |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | WILAYA | KATA | MTAA | JIRANI NA | |
| | | | | | | 1.<br>2. |

Saini ya Mzazi/Mlezi__________________________________Tarehe__________________

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
# SHULE YA SEKONDARI KIBWEHERI

**KIAMBATISHO B**

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi_____________________________________________________________

1. Nimesoma na kuelewa maelekezo yote na ninakubali kujiunga na shule hii.
2. Naahidi kwamba;
   a) Nitazingatia sheria zote za shule na kutimiza Maelekezo yote yaliyotolewa.
   b) Sitashiriki vitendo vyovyote vya hujuma na vilivyo kinyume na sheria za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.
   c) Nitatunza mali ya Umma ikiwa ni pamoja na majengo, samani, vitabu na vifaa vya Maabara.
   d) Nipo tayari kuchukuliwa hatua yoyote stahiki endapo nitakiuka maelekezo yaliyotolewa kwenye fomu hii.

Saini ya mwanafunzi______________________________Tarehe________________

**AHADI YA MZAZI**

Mimi____________________________ambaye ni Mzazi/Mlezi wa _______________________

Naaahidi kwamba;

a) Nitashirikiana na shule katika malezi ya mwanangu kwa kuhakikisha anatii na kufuata sheria na taratibu zote za shule.
b) Nitamwezesha mwanangu kufika shule kila siku za masomo ( na zingine zitakavyoelekezwa) kabla ya saa 1:00 asubuhi.
c) Ninaruhusu mwanangu achukuliwe hatua za kinidhamu kwa mujibu wa miongozo endapo atavunja mojawapo ya sheria/kanuni ana taratibu

Saini ya Mzazi/Mlezi_________________________Tarehe____________

HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
SHULE YA SEKONDARI KIBWEHERI

**KIAMBATISHO C.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**PRESIDENT'S OFFICE, REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**STUDENT'S MEDICAL CERTIFICATE**

To be completed by a Government officer and returned to the head of **Kibweheri** Secondary School, P. O. Box 90113 Dar Es Salaam

Date………………………

To the medical Officer

…………………………

…………………………

…………………………

Re: ………………………………………………………………………………………….

Please examine the student mentioned above and comment on his/her health by responding to the following items. Kindly put a tick or cross in front of either YES or NO as you find appropriate

1. Does student have problems in connection with

(a) Sight? (1) NO (2) YES
If yes,
State ……………………………………………………………………………………………..
………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………

(b) Hearing ? (1) NO (2) YES
If yes
State…………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………

( c ) Speech? (1) NO (2) YES
If yes
State…………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………

( d ) Blood Pressure ? (1) NO (2) YES
If yes
State…………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………

( e ) T.B? (1) NO (2) YES
If yes
State……………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

( f ) Any physical disability? (1) NO (2) YES

If yes
State……………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

2. Do you; therefore recommend the said student medically fit studentship at this school?
( 1 ) No ( if no please state reason) (2) YES
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
Reasons
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………….. ………………….
Name and signature of medical officer Date